# HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI

**MKOA WA ARUSHA**
**Barua zote ziandikwe Kwa:**
**Simu Na: +255 764 961 311**
**+255 759 682 793**
**+255 754 635 910**

**ENGUTOTO SEKONDARI**
**S.L.P 143**

**MONDULI**
**13/12/2023**

KUMB. NA: ENG/SS/F1.JOIN.INSTR./2024
**NDUGU MZAZI/MLEZI WA** ………………………………………………………….
SHULE YA MSINGI ……………………………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA ~ 2024"JOINING INSTRUCTIONS ").**

**1.0. UTANGULIZI:**

Ndugu Mzazi/Mlezi, ninayo furaha kukutaarifu kuwa, mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha 1~ 2024 katika shule ya sekondari ENGUTOTO. Nitumie nafasi hii, kukupongeza wewe na mwanao kwa kupata bahati hii, ambayo watu wengi wameikosa. **HONGERA NA KARIBU SANA** katika shule ya sekondari ENGUTOTO, kwa ajili ya kupata **ELIMU BORA**. Ni matumaini yangu kuwa, mwanao ataitumia nafasi hii vizuri kwa manufaa yake binafsi, familia na Taifa kwa ujumla.

Shule ya sekondari ENGUTOTO, ipo mjini MONDULI mkabala na kituo cha Mafuta GAPCO, ambacho pia ni kituo cha Mabasi maarufu kwa jina la "SHELI" kilichopo katika barabara kuu ya ARUSHA ~ MONDULI. Shule ya sekondari Engutoto, ni ya **BWENI** kwa Wavulana kwa kidato cha **1** hadi cha **6**.

**2.0. Shule itafunguliwa rasmi siku ya JUMAPILI tarehe 07/01/2024** na mwanafunzi anatakiwa afike siku hiyo saa **4:00 asubuhi** , akiwa na Fomu zote zilizoambatanishwa na barua hii, zikiwa zimejazwa kikamilifu na wahusika na kuzikabidhi shuleni wakati wa usajili. Hakikisha mwanao anaripoti shule ndani ya siku 14 baada ya kufunguliwa shule.

**3.0. Vifaa/Mahitaji ya lazima unayotakiwa kumkamilishia mwanao ni kama ifuatavyo:**

**3.1. SARE ZA SHULE.**

- **i.** Suruali 2 za heshima zenye marinda (2) rangi ya **DAMU YA MZEE(MAROON)**
- ii. Shati 2 za heshima rangi nyeupe mikono mifupi,
- iii. Viatu vya ngozi nyeusi vya kamba **SIO BUTI** na visiwe na kisigino kirefu,
- **iv.** Soksi rangi **NYEUSI**
- v. Mkanda mweusi wa kawaida usio na urembo.
- **vi.** Jezi ( bukta na T shirt ) rangi ya **KIJANI**
- vii. Raba /viatu vya michezo
- **viii.** Trak suti rangi **ya KIJANI**
- ix. Masweta rangi ya **DAMU YA MZEE( MAROON)** yenye shingo V, UFITO MWEUPE SHINGONI NA MIKONONI.
- x. Tshirt 2 za rangi ya **KIJANI** zisizo na maandishi au michoro au picha

***NB: Shule hii imechaguliwa Kitaifa kuendeleza michezo hivyo kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na nguo za michezo.***

## **VIFAA/MAHITAJI YA BWENI**

i. Suruali 2 rangi **KIJANI** kwa ajili ya Kanisani/Msikitini.
**ii.** Shuka mbili za rangi ya **KIJANI**
iii. Blanketi moja
iv. Ndoo ndogo mbili za maji
v. Mto mmoja
vi. Sanduku imara la bati lenye kufuli mbili
vii. T shirt 2 za rangi ya **KIJANI** zisizo na maandishi au michoro au picha
viii. Net ya kuzuiya mbu
ix. Godoro la futi tatu (**AINA YA TANFOM)**
x. Sabuni za kufulia na kuogea

**3.2. VYOMBO VYA CHAKULA:**

i. Sahani, kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula chake, vyombo hivyo visiwe vya plastiki. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuchangia vyombo wakati wa kula.

**3.3 VIFAA VYA DARASANI.**

**i.** Daftari kubwa 12, rula ndefu ( futi moja) kalamu za wino, penseli na mkebe wa **Hisabati ( Mathematical set)**

ii. Daftari 10 ndogo kwa ajili ya kufanya mazoezi ya masomo( Test)
iii. Mfuko (School bag) mzuri na imara kwa ajili ya kubebea vitabu na daftari za shule .
iv. Mwanafunzi aje na **RIMU MOJA SIZE YA A4 NYEUPE** kwa ajili ya kufanyia mitihani na mazoezi atakayopewa shuleni.

**NB:** Mara mwanafunzi atakaporipoti shuleni atafanya mtihani wa upimaji KKK ( kusoma, kuandika na kuhesabu ) ili kubaini uwezo wake wa Kitaaluma.

**AFYA:**

- Shule inatoa huduma ya kwanza tu kwa mwanafunzi anapougua; aidha huduma za matibabu zaidi zinapatikana Hospitali ya Wilaya
- Mzazi unapaswa kumlipia mtoto wako fedha ya **BIMA** ya mwaka mzima Tshs **6000/=** pamoja na **PASPOTI** moja kwa ajili ya kukata Bima ya kikundi,
- Hii itamsaidia apate matibabu kwa urahisi pale anapougua.
- Kama mwanafunzi ana BIMA ya afya aje nayo shuleni

**4.0. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:**

(i) Wizi wa aina yoyote,
(ii) Uasherati, Ubakaji, Ulawiti na Ushoga,
(iii) Ulevi na matumizi mabaya ya dawa za kulevya,
(iv) Uvutaji wa bangi,
(v) Makosa ya Jinai,
(vi) Kupiga au kupigana,
(vii) Kuharibu kwa makusudi mali ya mtu/shule /Umma/ mzazi atafidia gharama za uharibifu huo.
(viii) Kudharau bendera ya Taifa /Viongazi wa Serikali,
(ix) Kuoa

(x) Kutohudhuria vipindi vya darasani, ikiwa ni pamoja na vipindi viwili (2) vya Dini kila wiki, kutofanya mitihani, majaribio au kazi nyingine za shule bila kibali cha Mkuu wa shule.
(xi) Kugoma, kuchochea na kuongaza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule,raia na mali zao
(xii) Ushabiki wa vyama vya siasa ukiwa shuleni,
(xiii) Kuvunja sheria za shule.
(xiv) Kukataa adhabu ya viboko.
(xv) Ni marufuku mwanafunzi kuja na **SIMU YA MKONONI SHULENI**.
(xvi) Mwanafunzi atakaye miliki simu atafukuzwa shule


**Kaulimbiu ya shule ni "EDUCATION FOR WISDOM"** (ELIMU KWA AJILI YA KUPATA BUSARA)

**HITIMISHO:**

Ikiwa Mzazi/Mlezi na mwanafunzi HAKUBALIANI na MASHARTI yaliyotajwa katika maagizo haya, mwanafunzi ASIJE SHULENI na MZAZI/MLEZI afanye utaratibu wa kumtafutia UHAMISHO kijana wake kwenda shule nyingine itakayomfaa. Mwanafunzi anayeamua kuja hapa shuleni, baada ya kusoma na kuelekezwa taratibu za shule hii ya sekondari Engutoto, **hategemewi kuvunja Sheria / Kanuni na Taratibu za Shule**, kwani akifanya hivyo ni kwa makusudi na sio bahati mbaya.

"Ndugu Mzazi/Mlezi unakumbushwa kukamilisha mahitaji ya mtoto ya shule ili aripoti shuleni kwa tarehe husika. Mzazi/Mlezi atakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria kwa kumnyima mtoto haki yake ya msingi ya kupata elimu .Aidha iwapo utampeleka mwanao shule ya binafsi toa taarifa mapema kwa mkuu wa shule au katika ofisi ya Afisa Elimu sekondari ili kuepuka usumbufu wa kukamatwa."

Mwisho, Karibu sana Shule ya Sekondari ENGUTOTO ili ufaidike kwa kupata ELIMU BORA




**ISAYA MARTIN SWAI**
**MKUU WA SHULE**

**Nakala:**

- **Katibu Mkuu ~ WEMU …………………. Kwa Taarifa**
- **Mkurugenzi mtendaji H/shauri ya (w) monduli ……….kwa taarifa**
- **Afisaelimu (M) …………………. Kwa Taarifa**
- **Mkaguzi Mkuu wa Shule (K) ………………….. Kwa Taarifa**
- **Afisaelimu shule za sekondari (W) MONDULI ……… Kwa Taarifa**
- **Wajumbe wa Bodi ya Shule ~ Engutoto Sekondari ... Kwa Taarifa**
- **Faili la shule**

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI

**MKOA WA ARUSHA**
**Barua zote ziandikwe kwa:**
**Simu Na:+255 764 961 311**
**+255 759 682 792**
**+255 754 635 910**

**ENGUTOTO SEKONDARI**
**S.L.P 143**
**MONDULI**

**13/12/2023**

---

**TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI FOMU A**
**SEHEMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE KWA HERUFI KUBWA:**

1. (I) **JINA LA MWANAFUNZI** …………………………………………………
NB: Jina liwe lile lililotumika katika mtihani wa darasa la saba 2023.
(ii) Shule alipomaliza Elimu ya msingi………………………………
(iii) Tarehe ya kuzaliwa ………………… kijiji …………………… kata ……………
Tarafa ……………………….. Wilaya ……………………….. Mkoa……………
(iv) Dini ……………………………………… Madhehebu ……………………….

2. **AFYA:**
(i) Taja magonjwa yoyote makubwa uliyowahi kuugua k.m.f. TB, POLIO, KIFAFA n.k.
……………………………………………………………………………………………
(ii) Taja matatizo yoyote ya afya yako ………………………………………………..

**NB**: Wanafunzi wenye matatizo mbalimbali ya afya wahakikishe wanawasilisha vyeti vya Daktari pindi wanaporipoti shuleni.

3. **JINA LA MZAZI:**
(i) Baba …………………………………………. Hai/ Amefariki Lini …………....
(ii) Mama ………………………………………… Hai/ Amefariki Lini ……………….
(Kata isiyostahili)

4. **KAZI YA:**
(i) Baba ……………………… Dini ………………… Madhehebu …........................
(ii) Mama …………………….. Dini …………………. Madhehebu ………………….
(iii) Anwani ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………....
(iv) Mwanafunzi anaishi na: (Weka V sehemu iliyo sahihi)
(a) Baba tu (b) Mama tu
(c) Wazazi wote wawili (d) Mlezi

5. **MZAZI/MLEZI/TAASISI ITAKAYOGHARAMIA MAHITAJI YA SHULE:**

(i) Jina ……………………………………………………………………………….
(ii) Kazi yake ni …………………………………………………………………….
(iii) Anuani yake ni …………………………...... (iv) Simu ……………………………..
(v) Uhusiano wake …………………………. (Mf. Baba, Mama, Dada, Mjomba n.k)
(iv) Dini yake …………………………...... Madhehebu ……………………………….

6**. UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI:**

Mimi ……………………………….. nakubali kujiunga na Shule ya ENGUTOTO Sekondari na kuthibitisha kuwa, nitafuata sheria na Taratibu zote za Shule hii ili nitimize lengo la kuja shuleni kwa manufaa yangu/ familia na Taifa kwa ujumla. Endapo nitakwenda kinyume na Sheria /Kanuni /Taratibu za shule nitakubali kuadhibiwa.

Saini ya mwanafunzi ………………………………. Tarehe …………………………

# MONDULI DISTRICT COUNCIL

**ARUSHA REGION**

**TEL: Na: +255 764 961 311**
**+255 759 682 793**
**+255 754 635 910**

**ENGUTOTO SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX. 143**

**MONDULI**
**13/12/2023**

REF.NA.ENGU/SS/FI.JOIN.INSTR.2023/01

**TO: THE MEDICAL OFFICER,**

**PART A:**

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO:**
**MR/ ……………………………………………………… FORM I ~ 2024**

Please examine the above named as to his physical and mental fitness for full time schooling course. The Examination should include the following categories [i-iii].
Each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of a defect.

(i) (a) Eye
(b) Hearing
(c) Limbs
(d) Speech
(e) Venereal disease (s)
(f) Leprosy
(g) Epilepsy
(ii) Neuroses
(iii)Other serious disease

……………………………
ISAYA MARTIN SWAI
MKUU WA SHULE

HEADMASTER
ENGUTOTO
SECONDARY SCHOOL

**ISAYA MARTIN SWAI**
**HEADMASTER**

**PART B. MEDICAL CERTIFICATE**

[To be completed by Government Medical Officer]

I have examined the above named and consider that * he is physically * fit/unfit and mentally * fit/unfit for the full time schooling course:

(i). (a) Eye Sight ……………………………. (b) Hearing ………….....................
(c) Limbs ………………………………. (d) Speech ………………………….
(e) Venereal diseases (s) …………… (f) Leprosy ………………………..
(g) Epilepsy …………………………………..
(ii) Neuroses ……………………………………………………….
(iii) Other serious diseases …………………………………………

Station ………………………………………………. Signature ………………..............
Designation ………………………………………….. Date ………………………….

* Delete whichever is unnecessary.